

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**MKUTANO WA SABA
KIKAO CHA THELATHINI**

25 MEI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI – TAREHE 25 MEI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha

2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

258. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

- Je, ni lini Daraja la Mto Nduruma linalounganisha Kata za Mlangarini, Nduruma na Bwawani Wilayani Arumeru litajengwa.

259. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapandisha hadhi Shule ya Sekondari Kalenga iliyopo Kata ya Ulanda kuwa ya Kidato cha Tano na Sita.

**260. MHESHIMIWA ALLY YAHYA MHATA
(NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga Kituo cha Afya katika Kijiji cha Mikuwa Kata ya Mnanje Wilayani Nanyumbu.

**261. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA
(MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini mpango wa Serikali kufanya 50% ya Wanafunzi wanaojiunga Kidato cha Tano katika Shule za Kata watoke ndani ya Halmashauri.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**262. MHESHIMIWA MICHAEL COSTANTINO
MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-


Je, Serikali imejipangaje kuwaendeleza Vijana wanaomaliza Kidato cha Nne na kupata Daraja la nne au sifuri

WIZARA YA MADINI:

**263. MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY
MAGANGA (MBOGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, ni lini Serikali itawawezesha Wachimbaji wadogo kwa kuwapatia mikopo katika Wilaya ya Mbogwe.



WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**264. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA
THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara inayotoka Karagwe kupitia Nkwenda hadi Murongo itatengenezwa kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

**265. MHESHIMIWA MAULID ALI MOHAMED
(KIEMBE SAMAKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itakifanyia ukarabati Kituo cha Polisi Mazizini pamoja na kukarabati nyumba za Askari.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA
TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**266. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU
BUTONDO (KISHAPU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini Serikali itapeleka mawasiliano ya simu katika baadhi ya Kata Wilayani Kishapu.

WIZARA YA AFYA:

**267. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna Sheria ya Huduma ya Afya inayosimamia utoaji na upatikanaji wa huduma za afya.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**DODOMA
25 MEI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**